

BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1

Fax Nam. + 255 24 2230215

Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz



SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR

Barua Pepe: zahore@zanlink.com

TAARIFA YA SHUGHULI ZA MKUTANO WA TANO WA BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI UTAKAOANZA TAREHE 15 FEBUARI, 2017.

Mkutano wa Tano wa Baraza la Tisa la Wawakilishi Zanzibar unatarajiwa kuanza siku ya Jumatano tarehe 15 Febuari, 2017, saa 3:00 asubuhi.

SHUGHULI ZITAKAZOFANYIKA.

Shughuli za Mkutano huo zitakuwa kama ifuatavyo:-

1. Maswali na Majibu.

Maswali **112** yameratibiwa kwa ajili ya Mkutano huu na yanatarajiwa kujibiwa.

2. Miswada ya Sheria

Miswada ya Sheria iliyowasilishwa na kusomwa kwa mara ya Kwanza katika Mkutano wa mwezi Novemba, 2016 itasomwa kwa mara ya pili na kujadiliwa katika Mkutano huu wa Tano.

Miswada yenyewe ni:-

- i) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Nembo Nam. 1 ya 1985 na Sheria ya Bendera ya Zanzibar Nam.12 ya 2004 na Kutunga Sheria inayoweka Masharti Bora Yanayohusiana na Bendera ya Zanzibar, Nembo ya

Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar ya 2016 na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

- ii) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam. 9 ya 1992 na Kutunga Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Majukumu, Uwezo na Mambo Yanayohusiana na Hayo.
- iii) Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Namba 2 ya 2006.

3. Ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza kwa mwaka 2016/2017.

4. Hoja Binafsi ya Mheshimiwa Mohamed Said Mohamed Kuhusu Madawa ya Kulevya

(Raya Issa Msellem)
Katibu
Baraza la Wawakilishi
Zanzibar

13 Febuari, 2017